

**Rafiki Mpendwa,**

Tunatumaini jarida hili litakukuta mwenye afya njema wewe na familia yako. Wakati jarida hili lilipokuwa linaandikwa tulikuwa kwenye mwezi wa Ramadhani, ndio maana tunapenda kutuma salamu maalumu kwa marafiki zetu waislamu.

Kama unavyojua Oktoba 17 siku ya kuushinda umaskini uliokithiri duniani inakaribia. Kwa hiyo katika jarida hili tunaongelea zaidi kuhusu hili tukio na maandalizi yake. Kama kawaida tunaanza na shuhuda za baadhi ya marafiki. Wakati huu wanatuelezea kwa nini ni muhimu kwa wao kusherehekea Oktoba 17.

**Dear friend,**

We hope this Newsletter finds you and your family in good health. As this letter was written in the month of Ramadan we would like to extend special greetings to all our Muslim friends.

As you know, October 17<sup>th</sup>, the World Day to Overcome Extreme Poverty is approaching soon. As a result, we will speak especially about this event and its preparation in this newsletter. As usual we begin with the testimonies of some friends. They will explain to us why it is important for them to celebrate October 17<sup>th</sup>.

**“Kuwakomboa maskini, tuwafikilie”**

Alexs B. anaishi Ivory Coast, ni mtu maskini na mlemavu kutokana na vita. Baada ya kushiriki katika mkutano wa Oktoba 2007, alitumbia :

*“Hapa nimekaa karibu na waamuzi wa ngazi za juu kama mawaziri, maprofesa, madaktari nk. Nilikuwa na haki ya kuongea na nikasema sio vizuri kuwaongelea maskini wakati wenyewe hawapo. Nilisikilizwa na nilichosema kilizingatiwa. Waandaaji waliahidi wakati ujao watafanya chochote kinachowezekana ili wanaume na wanawake wenye historia ya umaskini watakuwepo. Hiyo inabadilisha kila kitu kwa sababu inamaanisha kwamba watu maskini wanaweza kufanya maamuzi yanayohusu nchi yao. Hiyo pia inamaanisha kwamba nchi haitajengwa na watu matajiri tu (...) Watu maskini lazima wafundishwe, lazima wajifunze kuongea mbele za watu ili waweze kuwasiliana na kila mtu. Kinachoweza kuwakomboa maskini ni kuwazingatia (...) Leo taratibu naanza kunyanzua kichwa changu juu.”*

*(imetolewa kutoka barua kwa marafiki duniani kote, Mei 2008)*

**“To liberate the poor, give them consideration.”**

Alexis B. lives in Ivory Coast. He is a poor person and displaced due to the war. After participating in a conference in October of 2007, he told us :

*“Here I am sitting next to high-level decision-makers, like government ministers, professors, doctors, etc. I had the right to speak and I said “it's not good to talk about poor people in their absence”. I was listened to and what I said was taken into consideration. The organisers promised that next time, they will do whatever is necessary so that men and women from very poor backgrounds will be present. That changes everything because that means that poor people can make decisions concerning their country. That also means that the country will not be built only with rich people (...). Poor people must be trained, must learn to speak in public so that they can communicate with everyone. What can liberate the poor is to give them consideration (...). Today, I am slowly starting to hold my head high.”*

*(extract from the Letter to the friends around the world, May 2008)*



ATD Fourth World Movement - P.O. Box 61786 - Dar es Salaam  
 mail : [atd.tanzania@gmail.com](mailto:atd.tanzania@gmail.com) - tel : 022 - 276 17 17  
 English website : [www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html)  
 Tovuti ya Kiswahili : [www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html)



*imetolewa  
na Alain  
Genin,  
wakati  
alipokuwa  
akiishi  
jamuhuri  
ya Afrika  
Kati*

*drawing by  
Alain  
Génin,  
when he  
was living  
in the  
Republic of  
Central  
Africa*

In the Republic of Central Africa, in 2008, eight people came from four different neighbourhoods of Bangui and participated in the preparation of the World Day to Overcome Extreme Poverty. In every preparation meeting, they expressed how important it was to gather and to live in unity in order to be efficient in the struggle against extreme poverty : **"Unhappiness to the man who thinks alone. A man alone can neither live nor build a country."**

Last year, Mama S. (from Tandale, a neighbourhood of Dar es Salaam) told us, when coming back from the October 17<sup>th</sup> celebration : **"What made me happy is to see how I am being valued : to be invited to the meeting and to be given a message to read in a crowd of very poor people and I am one of them."**

Katika Jamuhuri ya Afrika ya Kati, mwaka 2008, watu wanane kutoka maeneo manne tofauti ya Bangui na wakashiriki katika maandalizi ya siku ya kuepukana na umaskini uliokithiri duniani. Katika kila mkutano wa kuandaa walieleza jinsi gani ilivyomuhimu kukusanyika na kuishi kwa umoja ili kuwa madhubuti katika kupambana na umaskini uliokithiri : **"Huzuni kwa mtu ambaye hufikiri peke yake. Mtu peke yake hawezi kuishi wala kujenga nchi."**


In Europe October 17<sup>th</sup> is also celebrated every year. For a celebration in Ireland, Mr and Mrs E. coming from the UK declared : **"It is togetherness which marks the October 17<sup>th</sup>. (...) Togetherness is what we need to grow up, to be able to bring up our children. Togetherness gives us trust in ourselves and in others, to believe in each other."**

Mwaka jana Mama S, (kutoka Tandale, eneo la Dar es Salaam) alituambia tuliporudi kutoka katika sherehe za Oktoba 17 : **"Kitu kilichonipa furaha ni kuona jinsi gani nilivyojaliwa : kualikwa kwenye mkutano na kupewa ujumbe kuusoma mbele ya umati wa watu maskini na mimi nikiwa mmoja wapo."**

*Sherehe za  
Oktoba 17  
ya Cusco,  
Peru*

Ulaya vilevile wanasherehekea Oktoba 17 kila mwaka. Kwa sherehe ya Ireland, Bw na Bibi E. kutoka Uingereza walitamka : "Ni umoja ambao unaonesha Oktoba 17. (...) Umoja ndio kitu tunachohitaji kukikuza, kuweza kuwalea watoto wetu. **Umoja unatupa uaminifu kwetu na kwa wenzetu, kuaminiana."**

*October  
17<sup>th</sup>  
celebration  
in Cusco,  
Peru*





## Matembezi kuelekea Oktoba 17 ijayo ...

## Walking towards next October 17<sup>th</sup>...

Siku ya kuushinda umaskini uliokithiri itasherehekewa tarehe 17 Octoba kama kila mwaka katika nchi nyingi duniani kote.

Ndani ya ATD (Dunia ya Nne) siku hii itaunganishwa na sherehe ya Miaka 20 ya ukumbusho wa makubaliano ya haki za mtoto. Haya makubaliano yalisainiwa na Tanzania na nchi nyingi nyingine. Yanahusu haki nyingi kwa mfano haki ya kujitambua, haki ya kuishi na familia yake, haki ya elimu, n.k.

### **Tunapanga nini Dar es salaam?**

Dar es Salaam tangia Januari 2009 (kama ulivyosoma katika jarida letu la Juni 2009) Tunafanyia kazi haki ya elimu, Timu ya ATD imekusanya uzoefu wa baadhi ya wazazi ambao wanaishi katika maeneo maskini na vigumu kwa watoto wao kuingia shule ya msingi. Ndio maana mwaka huu sherehe za Oktoba 17 zitakuwa zinazungukia swali hili.

Kuandaa siku hii, tunaalika marafiki na mashirika kutoka Dar es Salaam kujiunga na sisi ili kusherehekea siku hii pamoja. Wengi wa hawa marafiki na mashirika tayari wamejiunga na watu wanaoishi katika mazingira magumu. Tunapenda siku hii iwe wakati maalumu kwa hawa watu wenye hali ngumu kuongea hadharani na kufanya wanavyovifanya ili watoto wao waende shule vijulikane na kuendelezwa. Tunafikiri ni muhimu sana jitihada zinazofanywa na hawa wazazi zifahamike na jamii na nchi. Mara nyingi hawa wazazi wanahusishwa sio tu na watoto wao bali pia na watoto wa maeneo hayo.

The World Day to Overcome Extreme Poverty will be celebrated on the 17<sup>th</sup> of October, like every year, in many countries throughout the world.

Within the ATD Fourth World Movement this day will be linked to the celebration of the 20<sup>th</sup> anniversary of the Convention on the Rights of the Child. This Convention has been signed by Tanzania and many other countries. It refers to a large number of rights, for example the right to an identity, the right to live with family, the right to education, etc.

### **What do we plan in Dar es Salaam ?**



*Mkutano wa maandalizi pamoja na wazazi katika kitangoji cha Dar es Salaam*

*Preparation meeting with parents in a Dar es Salaam neighbourhood*

Since January 2009 (see June 2009 Newsletter), the ATD team have been working on the right of education and have gathered the experience of parents who are living in poor neighbourhoods who have had difficulties having their children access primary school. That's why this year's October 17<sup>th</sup> celebration

will be concentrating on this topic.

In preparation of this day, we are inviting friends and associations from Dar es Salaam to join us in celebrating this day together. Most of these friends and associations are linked to people living in very difficult conditions. We would like this Day to be the occasion for these disadvantaged people to speak out publicly and to make known what they have to do to enable their children to go to school and to succeed. We think it is very important that the efforts of these parents are known by their community and by the country : very often these parents are involved not only in striving for an education for their for own children, but also for the children of their community.

## Unaweza kufanya nini hapo ulipo?

Kila mmoja, kila mwananchi anakaribishwa kusherehekea siku hii sehemu yoyote alipo, katika sehemu anayoishi au anayofanya kazi... Mwaka jana, katika jarida la mwezi wa Juni na Septemba 2008, tulishirikiana na nyie baadhi ya mawazo kuhusu nini kifanyike na kwa jinsi gani ! Kama unahitaji kusoma hizi nakala unaweza kuzipata kaitika [www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Kiswahili-.html) au tunaweza kukutumia. Usisite kutuuliza.

Kama kumbusho, mambo muhimu kwa kifupi katika hii sherehe :

- jaribu kukusanya watu maskini sana na wale wanaotengwa na wale wanaojihusisha na kupambana na umaskini uliokithiri,
- saidia watu maskini sana wawe na moyo na siku hii, waruhusu waongee kwa wazi (kwa mfano wacha waelezee wanafanya nini kuwapelekea watoto wafaulu shuleni),
- kumbusha historia ya hii siku, soma ujumbe uliochongewa katika jiwe la kumbukumbu katika uwanja wa haki za binadamu na uhuru Paris :

*“Popote pale wanaume na wanawake wanapohukumiwa kuishi katika umaskini uliokithiri haki za binadamu zimevurugwa.*

*Kuungana pamoja ili kuhakikisha kwamba hizi haki zinaheshimiwa ni jukumu letu sote.”*

Joseph Wresinski  
Mwanzilishi wa ATD Dunia ya Nne

- na vilevile : andaa kitu chochote kulingana na uwezo wako. (Tunaweza kukusaidia na ushauri na maandiko lakini hatuwezi kutuma pesa.)

## What can you do where you are ?

Everyone of us, every citizen, is invited to celebrate this Day wherever he or she is, in his or her living or working place. Last year, in the June and September 2008 Newsletters, we shared some ideas with you about what can be done and how to go about it. If you need to re-read these copies, you can find them at [www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html](http://www.atd-fourthworld.org/-Tanzania,549-.html) or we can send them to you. Don't hesitate to ask us.

As a reminder, the most important points for this celebration summarize as follows :

- try to gather very poor and excluded people and those who are involved in the struggle against Extreme Poverty,
- help the very poor people to be at the heart of this day, allowing them to speak out (for example letting them explain what they do to have their children succeed at school).
- remember the history of this day, reading the text engraved on the Commemorative Stone on the Plaza of Human Rights and Liberties, in Paris :

*“Wherever men and women are condemned to live in extreme poverty, human rights are violated.*

*To come together to ensure that these rights be respected is our solemn duty.”*

Joseph Wresinski,  
Founder of ATD Fourth World

- and of course : organise something according to your own means. (We can help you with advice and texts but we cannot send you any money.)

Tunakutakia wakati wa kukutana wenye furaha na mikusanyiko ya amani wakati wa kusherehekea Oktoba 17. Asante kwa kutuambia nini unapanga kufanya. Kama utatumia picha na shuhuda baada ya sherehe tunaweza tukazichapisha katika hii barua.

*Wako, Timu ya ATD Dunia ya Nne  
ya Dar es salaam.*

We wish you a time of joyful encounters and peaceful gatherings during your celebration of October 17<sup>th</sup>. Thank you for telling us what you are planning to do. If you send us some pictures and testimonies after your celebration we can publish them in this letter.

*Your ATD Fourth World Team  
in Dar es Salaam*